**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2015.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**-------------------------**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.1 Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

**1.2 Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake katika Bunge la Kumi, naomba nichukue fursa hii ***kukupongeza wewe binafsi na Ofisi ya Bunge*** kwa kufanya marekebisho katika Kanuni za Kudumu za Bunge na hatimaye **kuundwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**. **Tanzania iliihitaji kamati hii juzi na wala siyo jana! Bunge lako Mhe. Spika litakumbukwa kwa kuweka historia ya kubuni na kuanzisha Kamati hii nyeti.** Kuundwa kwa Kamati hii, kumelipa Bunge lako tukufu, nyenzo muhimu ya usimamizi wa utekelezaji wa sera na mipango ya serikali kwenye eneo nyeti la Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**1.3 Mheshimiwa Spika**, **ninadiriki kusema kwamba, katika miaka miwili na nusu ya uhai wake, Kamati ya**

**Bunge ya TAMISEMI, pamoja na eneo la kazi kuwa pana na kazi kuwa nyingi kuliko muda na idadi ya wajumbe, imejitahidi sana kutekeleza majukumu yake kwa tija na ufanisi wa hali ya juu**. Imeisimamia ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa weledi wa hali ya juu, lengo likiwa kuhakikisha Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinawahudumia wananchi kikamilifu kwa kuwaletea maendeleo wanayotarajia. **Bunge lako bado lina changamoto kubwa ya kuishawishi Serikali kuleta mabadiliko ya kimfumo na kiutendaji, ili kuondokana na utamaduni wa kuendesha dola kwa mazoea na badala yake Serikali ibuni namna bora, yenye tija na ufanisi, na zaidi inayoweza kupimika kirahisi, ili kufikia malengo ya kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi. Kamati ya namna hii kwenye Bunge lijalo inapaswa kufanya kazi *'muda wote'* ili ifike maeneo yote na kuzisimamia halmashauri ipasavyo. Tulichobaini ni kuwa bila usimamizi madhubuti wa taasisi ya Bunge, halmashauri hazifanyi kazi yake ipasavyo.**

**1.4 Mheshimiwa Spika**, **kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa, naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI kwa kuniamini, kunichagua mimi kuwa kiongozi wao na kwa kunipa ushirikiano niliostahili kwa kipindi chote cha uhai wa Kamati hii.** Sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wajumbe hawa mahiri kwa kuonesha weledi, utaalamu wa hali ya juu katika uchambuzi na upembuzi yakinifu wa masuala ya kisera katika sekta mbalimbali. Aidha,

niwashukuru kwa mahudhurio mazuri wakati wa vikao na kwa kujitolea kufanya kazi kwa saa nyingi. Hakika utumishi wao katika Kamati hii na Bunge lako tukufu, siku zote umekuwa ni wenye kutukuka, nami kiongozi wao nasema: nitauenzi daima.

Kwa umuhimu mkubwa, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. John Paul Lwanji, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu, Mb
4. Mhe. Highness Samson Kiwia, Mb
5. Mhe. Asha Mohamed Omari, Mb
6. Mhe. Rosweeter Faustine Kasikila, Mb
7. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mb
8. Mhe. Eugen Elishiriga Mwaiposa, Mb
9. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
10. Mhe. Mhandisi. Dkt. Athuman R. Mfutakamba, Mb
11. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
12. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
13. Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga, Mb
14. Mhe. Moses Joseph Machali, Mb
15. Mhe. Sylvester Massele Mabumba, Mb
16. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb
17. Mhe. Dkt. Mathayo David Mathayo, Mb

**1.5 Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Uchambuzi huo ulifanywa katika Vikao vya Kamati vilivyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam kati ya terehe 21 Aprili na 07 Mei, 2015. Katika kipindi hicho, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb) aliwasilisha taarifa kuhusu Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Taasisi zilizo chini yake. Aidha, Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara waliwasilisha Bajeti za Mafungu ya Mikoa (Regional Votes) kwa niaba ya Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

### 2.1 <u>Makusanyo ya Maduhuli</u>

2.1.1 **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake, Tawala za Mikoa na Halmashauri zilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya **Sh. 463,387,311,819**. Kamati ilipokea taarifa kwamba, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 makusanyo yalikuwa jumla ya **Sh. 299,405,579,805** sawa na wastani wa asilimia sitini na nne nukta sita moja (64.61%) ya malengo yaliyowekwa.

2.1.2 **Mheshimiwa Spika**, Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake ambazo ni Shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Mikopo ya Serikali za

Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI) na Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART) kwa pamoja zilikusanya wastani wa asilimia mia moja thelathini na mbili (132%) ya malengo yaliyowekwa. Kamati ilielezwa kwamba, pamoja na sababu nyingine, makusanyo yalizidi makadirio kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni za ununuzi na usambazaji wa vitabu na madawati kuongezeka kuliko ilivyotarajiwa hapo awali.

2.1.3 **Mheshimiwa Spika,** Sekretarieti za Mikoa kwa ujumla wake zilikusanya wastani wa asilimia nane (8%) tu ya malengo yaliyowekwa. Baada ya kufanya uchambuzi katika randama za mikoa yote ya Tanzania Bara, Kamati ilibaini kwamba, wastani wa makusanyo madogo ya Tawala za Mikoa unasababishwa na baadhi ya sekretarieti za mikoa kutokusanya kabisa, baadhi kujiwekea malengo madogo ya makusanyo au/na kukusanya chini ya malengo.

2.1.4 Kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, makusanyo yalikuwa wastani wa asilimia sitini na nne (64%) ya malengo yaliyowekwa. Kwa wastani, kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na matarajio ya makusanyo kufikia Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha. Katika uchambuzi uliofanywa na Kamati, ilibainika kwamba baadhi ya halmashauri zilikusanya kikamilifu na kufikia matarajio na kukusanya zaidi ya asilimia sabini na tano (75) ya makisio kufikia Machi, 2015. Kamati inazipongeza Halmashauri za Mkoa wa Lindi ambazo kwa ujumla wake wastani wa makusanyo katika vyanzo vya ndani *(own source)* ulikuwa asilimia tisini na moja

(91%) ya malengo waliyojiwekea na hivyo kuonesha mfano kwamba, tukiamua kukusanya kutoka katika vyanzo vyetu vya ndani, tunaweza.

2.1.5 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa kuna changamoto nyingi katika eneo la makusanyo yatokanayo na vyanzo vya ndani. Baadhi ya changamoto hizo ni mwingiliano wa kisheria na kimamlaka baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika ukusanyaji kutoka katika vyanzo vilivyopo katika halmashauri. Kwa mfano, Sheria ya Utalii ya Mwaka 2008[1] ilifuta ushuru wa hoteli ambao ulikuwa unakusanywa na halmashauri hapo awali.

2.1.6 **Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine ni Serikali kuu kutozingatia baadhi ya matakwa ya kisheria na kimakubaliano juu ya asilimia ya makusanyo yanayostahili kubaki katika Serikali za Mitaa kutokana na kodi zinazotozwa katika sekta mbalimbali kama vile asilimia ishirini na tano (25%) ya kodi ya uwindaji, asilimia tano (5%) ya thamani ya mauzo ya mazao ya misitu na asilimia thelathini (30%) ya kodi ya ardhi zinazopaswa kurudishwa katika halmashauri baada ya kukusanywa. Uzoefu unaonesha kuwa Wizara husika na Hazina zimekuwa hazirejeshi fedha hizo kikamilifu.

2.1.7 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, halmashauri nyingi zinakosa mapato yatokanayo na mauzo ya chakula kwa kuwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) umekuwa haulipi fedha zitokanazo na mauzo ya mazao ya chakula. Kasoro hii

[1] Sheria Na. ... ya Mwaka 2008

pia inajitokeza katika ukusanyaji wa ushuru wa mazao mengine ya biashara ambapo makusanyo hufanywa na bodi zinazosimamia mazao hayo kama Bodi ya Kahawa, Bodi ya Pareto na Bodi ya Pamba.

## 2.2 Mtiririko wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

2.2.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa kuwa hali ya mtiririko wa fedha za mishahara na stahili za watumishi ilikuwa nzuri kama ilivyotarajiwa kufikia Machi, 2015. Hata hivyo, hali ya mapokezi haikuwa nzuri kwa upande wa fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Taasisi zake, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri, kwa pamoja zilipokea wastani wa asilimia arobaini na mbili (42%) ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge.

2.2.2 **Mheshimiwa Spika,** kwa sehemu kubwa, kutotolewa kikamilifu na kwa wakati kwa fedha za Matumizi Mengineyo, imekuwa ni changamoto kubwa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa sehemu kubwa kumekwamisha utekelezaji wa mipango ya kibajeti iliyowekwa. Katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 halmashauri nyingi zilipokea kiasi kidogo cha fedha za ruzuku ya fidia kwa ajili ya matumizi ya kawaida (GPG) na kwa sababu hiyo, Kamati imebaini kwamba, halmashauri hizo zimekuwa zikitumia kiasi kikubwa cha fedha zitokanazo na makusanyo ya ndani *(own source)* kugharamia matumizi mengineyo.

## 2.3 Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo

2.3.1 **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliidhinishiwa jumla ya Sh. 1,179,858,915,000[2] kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo *(development budget)* ikijumuisha fedha za ndani na fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 hali ya mtiririko wa fedha haikuwa nzuri ukilinganisha na bajeti iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa mtiririko wa fedha ulikuwa kama ifuatavyo:-

a) Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na taasisi zake ilipokea jumla ya Sh. 234,177,167,158 kati ya Sh. 431,657,767,000 iliyoidhinishwa, sawa na asilimia hamsini na nne (54%);

b) Tawala za Mikoa zilipokea kiasi cha Sh. 12,053,071,824 kati ya Sh. 65,599,104,000 zilizoidhinishwa, sawa na wastani wa asilimia kumi na nane (18%);

c) Halmashauri zilipokea kiasi cha Sh. 160,145,990,789 kati ya Sh. 682,602,044,000 zilizoidhinishwa, sawa na wastani wa asilimia ishirini na tatu (23%).

2.3.2 **Mheshimiwa Spika**, mtiririko finyu wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, hususan katika halmashauri, si tu unakatisha tamaa wananchi ambao wanatarajia kupata huduma za msingi kutoka katika Serikali, lakini haioneshi nia ya dhati ya Serikali katika kuwaletea wananchi hao maendeleo. Kamati imebaini kuwa, mapokezi ya fedha za wadau wa maendeleo

[2] Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2015/2016 Uk. 5 - 8

katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 nayo ilikuwa ya kusua sua kwa sababu mbalimbali.

2.3.3 **Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati ikifanya ziara katika mikoa mbalimbali kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ilishuhudia miradi mingi iliyopangwa kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kutoanza kutekelezwa au kutekelezwa kwa kuchelewa. Sababu kubwa iliyotolewa ni kutotolewa kikamilifu kwa fedha kutoka Serikali Kuu. Kwa mfano, Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani iliyoko Tumbi, Kibaha, ulitengewa kiasi cha **Sh. 1,000,000,000/=** katika Bajeti ya 2014/2015 kati ya mahitaji Halisi ya Mradi huo ya **Sh. 6,000,000,000/=**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Mradi huo ulikuwa umepokea **Sh. 600,000,000/=** tu.

2.3.4 **Mheshimiwa Spika, kamati imesikitishwa sana na muendelezo wa serikali kutunga bajeti za namna hii, zisizotekeleka na zisizoleta mabadiliko, na imeshangazwa zaidi kuona bado serikali inaendelea kutumainia fedha toka kwa wahisani na wabia wa maendeleo. Tunahoji: ni lini serikali itatoka kwenye usingizi huu mzito? Na zaidi kamati, imeshangazwa kuona hata mwaka huu maombi ya fedha za bajeti bado yana mkono wa wahisani ndani yake. Kamati inahoji, ni lini nchi yetu itaamua kujitegemea kwa vitendo? Ni kwa nini tusipange bajeti yetu kwa kutazama kidogo tulichonacho ndani ya nchi tu? Na kuacha fedha**

**za wahisani zibaki kuwa za nyongeza, nje ya umbile la bajeti?**

2.3.5 **Mheshimiwa Spika,** kamati yangu inaamini kwamba, **ni kwa kujitegemea tu ndo tutaona tija na ufanisi kwenye kukusanya mapato na ndipo tutaona umuhimu wa kuwa na nidhamu ya matumizi, ni kwa kuamua kujitegemea tu ndipo tutaona umuhimu wa kupunguza ukubwa wa serikali na kubana matumizi, ndipo tutaona umuhimu wa kukuza ajira kwenye sekta binafsi kwa kuwezesha na kuhamasisha uwekezaji wa watu binafsi ili baadae tuwadai kodi ya Jamhuri, ndipo tutaona umuhimu na ulazima wa kutanua wigo wa kodi na kupunguza misamaha ya kodi. Tukiendelea kutegemea misaada kutoka kwa wahisani kamwe tusijidanganye tutakuja siku moja kuendelea.**

2.3.6 **Hakuna nchi hapa duniani iliwahi kujengwa na watu kutoka nchi nyingine, kwa mitaji na pesa kutoka nchi nyingine, maana hawa huondoka na faida, raslimali na mitaji yao – wamewahi kuacha nini Tanzania toka waanze kuja kuchimba dhahabu zetu? Ni lazima mzunguko na njia kuu za uzalishaji zimilikiwe na wenye nchi ndipo sasa utaona uchumi wa nchi ukiimarika.**

2.3.7 **Dambisa Moyo anasema kwenye kitabu chake cha *Dead Aid*, kuwa misaada kutoka kwa wahisani kwa kiasi kikubwa badala ya**

**kuiwezesha Afrika kukua kiuchumi, imesaidia Afrika kudumaa na kushindwa kufikiria nje ya boksi, na anahitimisha kwa kusema kuwa misaada hiyo ni misaada ya kifo na kwa maana hiyo kuna kila sababu ya nchi za Afrika kuamka na kufikiria upya.**

2.3.8 **Sababu za kukosa fedha kwa ajili ya maendeleo zinajulikana; kubwa ikiwa ni matumizi makubwa ya serikali, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya pesa zote inaelekezwa kwenye matumizi ya kawaida na chini ya asilimia 20 tu ndo inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo. Hivi hii ingekuwa biashara, tujiulize, hii kampuni ingesimama kweli? Haya matumizi ya kawaida yanaenda kufanya shughuli zipi kama hakuna pesa za maendeleo? Tunalipa mishahara kwa wafanyakazi na kugharamia magari yao, vikao vyao, mafunzo yao na mengineyo ili wakatekeleze mpango gani na kwa kutumia fedha zipi? Maana hata kwenye hizo kidogo zinazopangwa, zinazoenda kwenye mamlaka za serikali za mitaa ni hizo (mfano kwa mwaka wa fedha unaoisha, asilimia 23 tu!). Hivi nikisema kodi ya watanzania inatumiwa bila faida inayostahiki kwa asilimia 99 ya watanzania, na watumishi wa Serikali asilimia 1 tu nitakuwa nimekosea?**

2.3.9 **Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali itazame namna mpya ya kupanga bajeti ili iweze kujijengea uhalali kwa wananchi, kuwa ni kwa**

**nini inaomba bajeti yake. Mfano, kama kwenye wilaya kuna majengo 17 ya zahanati yaliyojengwa na wananchi miaka zaidi ya 7 iliyopita na kukamilishwa mpaka hatua ya boma yakisubiri serikali iyamalizie, na hayajamaliziwa kwa sababu hakuna pesa zinazoenda, wale watumishi wa serikali za mitaa kwenye wilaya hiyo wana uhalali gani wa kuendelea kuwepo ofisini na kulipwa mishahara yao? Na serikali inapata uhalali gani wa kuendelea kutuma pesa za matumizi mengineyo kama hakuna pesa za miradi ya maendeleo? Watumishi wa umma wanaendelea kulipwa haki zao bila wao kuleta mabadiliko kwenye maisha ya wananchi, ni lini unadhani watashtuka na kuchukua wajibu wa kulitumikia Taifa kwa kujitoa zaidi? Hivi hata wanaiona *'privilege'* waliyopewa na Jamhuri?**

## 2.4 Utekelezaji wa Maoni/Maagizo ya Kamati

2.4.1 **Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Mwaka 2014/2015, Kamati ilitoa maoni mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi[3]. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa, ushauri na maoni ya Kamati ulizingatiwa isipokuwa katika maeneo yafuatayo:-

[3] Tazama Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2014/2015

a) **Kutengwa kwa asilimia kumi (10%) ya bajeti ya makusanyo ya ndani (own source) kuwezesha vijana na wanawake**

Hili ni agizo litokanalo na Serikali yenyewe katika miongozo ambayo iliitoa siku za awali. Hata hivyo, halmashauri nyingi zimekuwa hazitekelezi agizo hili na hivyo kusababisha makundi haya kukosa uwezeshaji uliotarajiwa.

b) **Halmashauri kutenga asilimia isiyopungua sitini (60%) ya fedha itokanayo na makusanyo ya ndani (own source) kutekeleza miradi ya maendeleo**

Agizo hili halikutekelezwa kikamilifu kwa kiwango kilichokusudiwa na Kamati. Aidha, baadhi ya Sekretarieti za mikoa ambazo kwa mujibu wa maelekezo ya Kamati na kwa mujibu wa wajibu walionao kibajeti, hawakufanya ufuatiliaji wa kuzisimamia halmashauri na kuhakikisha agizo hili linatekelezwa.

## 2.5 Tathmini pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa Mwaka 2014/2015

2.5.1 **Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilibaini kwamba, kwa sehemu kubwa, bajeti iliyopangwa haikuzaa matunda yaliyotarajiwa. Kamati inaamini,

kutofikiwa kwa malengo tuliyojiwekea, kumesababishwa na sisi wenyewe kama Taifa kutotambua vipaumbele vyetu ni vipi au kama tunavitambua, kutovizingatia.

2.5.2 Aidha, Kamati imebaini kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kumekuwepo na makusanyo yasiyoridhisha katika Halmashauri nyingi ambayo kwa sehemu kubwa yamesababishwa ama na udhaifu katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vilivyopo au makisio ya chini katika bajeti ya makusanyo ya ndani. Kila mwaka tunajiwekea malengo ya makusanyo hususan katika vyanzo vilivyopo, lakini bado tumekuwa hatufikii malengo hayo. Inawezekana, hakuna tathmini ya uhakika kuhusu vyanzo vilivyopo na uwezo wa watendaji wa Serikali kukusanya kutoka katika vyanzo hivyo.

2.5.3 **Mheshimiwa Spika,** eneo lingine ni kukosekana kwa nidhamu ya matumizi ya fedha kwa mujibu wa bajeti iliiyoidhinishwa na Bunge na kutofuata mpango wa Bajeti. Kumekuwepo na tabia miongoni mwa taasisi za Serikali kujibadilishia matumizi ya fedha mara kwa mara bila kuzingatia vipaumbele tuilivyojiwekea au hata bila kulishirikisha Bunge pale inapobidi. Nidhamu hii, sio tu inatufanya kutokuwa watekelezaji wa Bajeti tunayojiwekea, bali itatufanya tuwe watumiaji wa kile kinachopatikana pale kinapopatikana.

2.5.4 **Mheshimiwa Spika**, Kamati bado inaamini kwamba, halmashauri zetu ndio mamlaka ya mwanzo kabisa katika kulipatia taifa letu mapato yatokanayo na makusanyo, mdau wa kwanza katika kujenga miundombinu ya kiuchumi, na ndio mdau mkuu katika

kulisogeza gurudumu la maendeleo kwa umma. Katika halmashauri kuna rasilimali watu kubwa zaidi na ndiko kwenye fursa nyingi za kiuchumi na kiuwekezaji.

## 3.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 3.1 Makadirio ya Mapato na Matumizi

3.1.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaomba kuidhinishiwa takriban **Sh. 5,452,020,389,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Makao Makuu), Tawala za Mikoa na katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo, **Sh. 4,303,103,822,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na **Sh. 932,741,708,000** ni kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la asimilia ishirini na moja (21%) ukilinganisha na bajeti ya Mwaka 2014/2015.

3.1.2 **Mheshimiwa Spika,** pamoja na masuala mengine, fedha inayoombwa imekusudiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

a) Kuziwezesha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia dhana ya kupeleka madaraka kwa umma;

b) Kujenga uwezo kwa watumishi wa Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa na Halmashauri kwa kuwapatia vitendea kazi na mafunzo mbalimbali ili waweze kuongeza ufanisi kazini;

c) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya mikoa na wilaya mpya zilizoanzishwa;

d) Kuendelea na ukamilishaji wa miradi yote iliyokwishaanza hususan ujenzi na ukarabati wa ofisi na nyumba za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na hospitali za mikoa ;

e) Kuboresha na kuongeza mtandao wa barabara vijijini; na

f) Upangaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo inayohusiana na sekta mbalimbali katika maeneo yao pamoja na miradi ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN)

## 3.2 Makusanyo ya Maduhuli

3.2.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa makusanyo**,** Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Taasisi zake, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri kwa pamoja zimekadiria kukusanya **Sh. 529,760,580,308** ikiwa ni ongezeko la asilimia kumi na nne (14%) ya makadirio ya makusanyo ya mwaka 2014/2015.

3.2.2 **Mheshimiwa Spika**, makusanyo hayo yanatarajiwa kuwa yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na

marejesho ya mishahara. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatotakana na kodi na ushuru mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vinavyotambulika kwa mujibu wa sheria.

## 3.3 <u>Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016</u>

**Makusanyo ya Maduhuli**

3.3.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa bado kuna changamoto kwa Halmashauri kuendelea kutegemea vyanzo vile vile vya mapato mwaka hadi mwaka. Endapo kunatokea jambo linaloathiri chanzo kimojawapo, makusanyo ya halmashauri hizo hushuka. Kamati inazishauri Halmashauri zote nchini kufanya utafiti wa kina *(economic baseline study)* kubainisha vyanzo vya mapato na uwezo wake ili Halmashauri hizo ziandae makadirio kulingana na uwezo wa ukusanyaji. Aidha, zihakikishe kuwa mikakati madhubuti inawekwa ili kukusanya mapato na kufikia malengo yatakayowekwa kwa wakati. Aidha, kwa mara nyingine na kwa msisitizo kwa sababu ya umuhimu wake, Kamati inazitaka Sekretarieti za Mikoa yote ya Tanzania Bara kuhakikisha kwamba inasimamimia zoezi hili kikamilifu.

3.3.2 **Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati imebaini kwamba, kukosekana kwa mapato kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa

usimamizi na ufuatiliaji na pia kuwepo kwa udanganyifu katika makusanyo unaochangia kupotea kwa mapato. Ni vyema Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Sekretarieti za Mikoa zikaimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji inayoleta matokeo yanayoonekana.

3.3.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, kuna baadhi ya vyanzo vya mapato katika Halmashauri vilifutwa, vingine mapato yake kuchukuliwa na Wizara Mama za Kisekta na nyingine kutegemea hali ya uzalishaji kama vile mazao ya chakula na mengine. Kwa sababu ya changamoto ya upatikanaji wa fedha za makusanyo ya vyanzo hivyo, Kamati inashauri kuwa, Halmashauri kukusanya kikamilifu katika vyanzo vyote vyenye uhakika.

3.3.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa na Bunge lako tukufu mwaka 2012 katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 kupitia Sheria ya Fedha Namba 8, Halmashauri zimewekewa mazingira mazuri zaidi ya ukusanyaji wa ushuru wa huduma *(service levy)* kama ifuatavyo:-

a) Sheria imeongeza wigo wa walipa ushuru ambapo wafanyabiashara wenye makampuni na wale wasio na makampuni *(corporate and non corporate entities)* wanatakiwa kulipa ushuru huo;

b) Matawi ya makampuni yanatakiwa kulipa ushuru huo kwenye Halmashauri ambako shughuli zake hufanyika.

Kwa msingi huo, Kamati inaziagiza Halmashauri zote nchini, kuhakikisha kuwa zinakuwa na Sheria Ndogo *(by-laws)* kwa madhumuni ya kutoza ushuru huo kikamilifu. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuzisimamia sheria, kwani moja kati ya tatizo kubwa linalozikabili sekta nyingi za umma, ni kutosimamia maamuzi na mikakati waliyojiwekea na hivyo kusababisha kutifikiwa kwa malengo yaliyowekwa.

3.3.5 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara husika katika sekta ya mawasiliano, itengeneze mfumo madhubuti wa kuhakikisha kuwa kodi ya minara ya simu inarejeshwa na kukusanywa na Halmashauri zote.

3.3.6 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya majengo *(property tax)* katika majiji, manispaa, miji na miji midogo kwani fedha nyingi zinapotea kwa kutokusanywa kikamilifu kwa kodi hii. Aidha, Serikali ifanye mabadiliko ya sheria kwa kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi hii ili iweze kutozwa kwa nyumba na majengo ambayo hayako katika maeneo ya majiji, manispaa, miji na miji midogo lakini yana hadhi na thamani inayostahili kutozwa kodi hiyo.

3.3.7 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inazitaka Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba zinawashirikisha wananchi kikamilifu katika maandalizi ya bajeti zao hususan katika mipango yote ya maendeleo, katika kubuni vyanzo vya mapato na pia katika utungaji wa sheria ndogo za ukusanyaji. Hatua hii itarahisisha zoezi la makusanyo bila manung'uniko.

Aidha, ushiriki wa wananchi utasaidia katika zoezi zima la kuchangia utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa pale ambapo Serikali kuu pamoja na Serikali za Mitaa zitakapokuwa zinatoa mchango wake kikamilifu katika miradi husika.

3.3.8 **Aidha kamati inaitaka serikali kuacha mara moja tabia ya kuwabana watu wenye kipato kidogo kwa kuwapandishia kodi na ushuru mwingine, makundi kama bodaboda, mama lishe, wamachinga, madereva taksi, na kuwapa misamaha ya kodi wanaovuna dhahabu na madini ya vito, wanaozalisha mafuta ya kula na wanaokuja kuwekeza kwenye uvunaji wa gesi. Hii ni aibu – kupambana na mnyonge na kumkimbia tajiri! Wana faida gani wawekezaji wanaokuja kuvuna rasilimali za nchi kwa gharama nafuu na wakaondoka na faida zao (na mitaji yao) na wakiwa matajiri zaidi kuliko walipokuja?**

## Mapato na Matumizi

3.3.9 **Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa, Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ujumla wake na hususan maafisa masuhuli wote, kuhakikisha kuwa wanatumia fedha zinazopatikana kwa kuzingatia vipaumbele vya kibajeti. Aidha, malipo mbalimbali yafanyike kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Fedha ili kupunguza uzalishaji wa madeni ya Watumishi na Wazabuni.

3.3.10 **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha kuwa nguvu kazi ya taifa inatumia fursa za kiuchumi zilizopo, Kamati inatoa agizo kwamba, Halmashauri zote nchini zihakikishe kuwa, **asilimia kumi (10%) itokanayo na mapato ya makusanyo ya ndani *(own source)* kwa mujibu wa maelekezo yaliyopo, inatengwa mahsusi kwa ajili ya kuwawezesha vijana na wanawake katika kuchochea juhudi za kujikwamua kiuchumi. Makundi haya ya kijamii ni muhimu sana katika ustawi wa jamii na kwa sababu hiyo, ni muhimu agizo hili lizingatiwe kikamilifu katika halmashauri zote.**

3.3.11 **Mheshimiwa Spika**, **Kamati inaendelea kuweka msisitizo kuhusu maelekezo yake kwamba, halmashauri zote zitenge asilimia isiyopungua sitini (60%) ya fedha itokanayo na makusanyo ya ndani *(own source)* baada ya makato ya asilimia kumi (10%) kwa uwezeshaji wa vijana na wanawake.** Asilimia hii ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo utokanao na agizo hili ujikite katika miradi inayoonekana *(tangible projects)* na ambayo inatatua matatizo ya kila siku ya mwananchi wa kawaida. Kamati inashauri kipaumbele kiwekwe katika upatikanaji wa huduma bora zaidi za msingi kwa wananchi, kama vile afya, elimu na maji.

3.3.12 Agizo hili lina malengo ya kuhakikisha kwamba, watendaji wa halmashauri wanaongeza juhudi katika kukusanya mapato na kuziba mianya ya ubadhirifu wa fedha za miradi ya maendeleo. Kamati inaamini

kwamba, hatua hiyo itaziwezesha halmashauri zetu kuanza kujiondoa taratibu katika utegemezi wa ruzuku kutoka katika Serikali Kuu katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Hali hii itaifanya nchi yetu kwa ujumla kupunguza na kuondokana na utegemezi wa misaada ya wadau wa maendeleo katika siku zijazo *(a simple strategic move to donor funds independency)*.

3.3.13 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Sekretarieti za Mikoa ziimarishe mfumo wa ufuatiliaji kwa kuzisimamia Halmashauri na kuhakikisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zitokanazo na makusanyo ya ndani pamoja na zile ambazo zinatoka nje zinatumika kuwaletea wananchi maendeleo, kwa wakati na kwa viwango stahiki na thamani ya fedha iweze kuonekana. Agizo hili linatokana na ukweli kwamba, Kamati inaamini kuwa wajibu wa kwanza wa usimamizi wa Halmashauri unaangukia mikononi mwa Tawala za Mikoa.

## 3.4 Maoni ya Jumla

### Umbile la Bajeti

3.4.1**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016[4], Bajeti inakadiriwa kuwa Sh. **Trilioni 22.48. Kati ya fedha hizo, Sh. Trilioni 5.45 zitatumika kwa ajili ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), sawa na 24.7% ya**

[4] Maelezo ya Waziri wa Fedha kwa Waheshimiwa Wabunge Kuhusu Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2015/2016 Uk. 17

**Bajeti Kuu. Kati ya fedha hizo, Sh. Trilioni 4.3 sawa na 78.9% ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Sh. Bilioni 932 sawa asilimia 21.1% ya Bajeti ya Ofisi hiyo ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.**

3.4.2 **Tujiulize kitu hapa, kama TAMISEMI kuna sekta zote zinazohusu maisha ya watanzania, na hii ndiyo share yake kwenye keki ya Taifa, hizo Wizara nyingine za kisekta, tukiondoa vyombo vya ulinzi na usalama na mambo ya nje, wanafanya nini huko? Kwa ajili ya nani? – na hizo asilimia zaidi ya 75 ya keki hii? Hii ni food for thought tu.**

3.4.3 **Mtazamo wetu ni kuwa tuna kila sababu kufikiria upya muundo wa serikali yetu na namna tulivyoyagawanya majukumu. Mfano, hivi kuna sababu gani ya kuwa na Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji – isiyowekeza wala isiyowezesha, maana kuna EPZA na TIC wanafanya kazi hiyo (na kwanza kuna haja gani ya kuwa na taasisi mbili zinazofanya kazi inayoshabihiana? Moja iko Wizara nyingine, na nyingine ipo Wizara nyingine), Wizara ya Viwanda na Biashara – isiyojenga viwanda wala isiyofanya biashara, maana siku hizi serikali haifanyi biashara; Wizara ya Maendeleo ya Jamii – isiyoendeleza jamii, maana watu wapo halmashauri na ndipo kwenye mfuko wa pesa za wanawake na vijana; Wizara**

**ya Kazi na Ajira – isiyozalisha ajira, maana wakulima na ardhi vipo halmashauri na wanaozalisha ajira ni aidha serikali yenyewe ama wajasiriamali wanaojiajiri na kuajiri wengine.**

3.4.4**Kwa mfano, kuna sababu gani ya kuwa na Wizara za Afya, Elimu, Kilimo, Maji, Ardhi n.k. wakati Hospitali, Shule, Mashamba, Viwanja/Ardhi vimepelekwa kwenye mamlaka za serikali za mitaa? Tutaambiwa, Wizara hizi za kisekta zinatunga sera – kwani kule TAMISEMI hawawezi kutunga sera?**

3.4.5**Mheshimiwa Spika, kusema ukweli, bila ulazima sana serikali yetu imejitwisha mzigo mzito sana wa mawizara na matokeo yake kukuza matumizi yake kuyahudumia mawizara haya kiasi kwamba halmashauri ambapo kuna watu, tunapumulia mashine; miradi midogo midogo tu kama ya kumalizia zahanati, nyumba za walimu na kuchimba visima haifanyiki!**

**Wengine tumekuwa tukihoji, hivi kulikuwa na haja gani kupeleka madaraka mikoani na hapo hapo kubakisha mawizara yote haya? Nadhani tunahitaji kulifanyia tafakuri tunduizi suala hili. Kwa kuwa huu ni mwaka wa mabadiliko, kuna kizazi kipya kinakuja na majibu ya masuala kama haya, basi na kipewe fursa tu.**

3.4.6**Mheshimiwa Spika, kwa mtiririko wa fedha za maendeleo ambao tumeushuhudia katika miaka michache iliyopita na Mwaka wa Fedha**

**2014/2015, hata kile kidogo kinachopangwa kutekeleza miradi ya maendeleo huwa hakipatikani kwa ukamilifu. Ni vema Serikali ikabadili mfumo wa kififikra katika kubajeti kulingana na uwezo tulio nao na pia katika kukusanya mapato ya ndani ili kuchochea maendeleo kwa wananchi ambao kodi yao ndiyo inatulipa mishahara na matumizi mengineyo.**

3.4.7 Pamoja na hayo, Serikali kuu ina wajibu wa kuhakikisha kuwa inapunguza matumizi yake, sio kwa maneno tu bali kwa vitendo ili fedha iliyopo iweze kukidhi mahitaji ya lazima ya Watumishi waliopo na watakoajiriwa. Aidha, Serikali ihakikishe kunakuwa kuna uwiano wa haki katika fedha zinazopelekwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayogusa wananchi wa kipato cha chini au wasio na kipato kabisa. **Kamati inaamini ni bora nchi ikawa na Bajeti ndogo inayotekelezeka kuliko kuwa na bajeti kubwa isiyotekelezeka.**

3.4.8 **Mheshimiwa Spika, kamati inalishauri Bunge lako tukufu litoe maagizo mahsusi kuhusiana na madeni ya walimu na watumishi wengine, pia madeni ya wazabuni waliokwisha toa huduma kwa serikali za mitaa.**

3.4.9 **Mheshimiwa Spika, kamati pia inarudia kutoa ushauri kwa serikali kuhusiana na wazo la kutengeneza mfumo wa motisha kwa watumishi wa sekta ya afya, kilimo, elimu na utawala wanaofanya kazi vijijini kwenye mazingira ya mbali na magumu. Hii itasaidia kuwabakiza kwenye maeneo hayo na kupunguza kiu ya**

**watumishi hawa muhimu kuhamia mijini ama kuishi mijini na kwenda kufanya kazi kijijini kwa muda mfupi tu na siku nyingine kutokwenda kabisa.** Mfumo wa mafao ni lazima uzingatie mambo ya makazi ya watumishi hawa, uwepo wa umeme kwenye maeneo haya, uwepo wa mawasiliano ya simu na intaneti sambamba na uwepo wa posho maalum ya kijiografia (inayolipwa kulingana na umbali kutoka kwenye mji). Hii italeta usawa (equity) kati ya maeneo ya vijijini na mijini katika ubora wa huduma nyeti zinazotolewa na serikali.

**Matumizi Bora ya Ardhi**

3.4.10 **Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, kwa kutambua mahitaji ya ardhi kwa wananchi, halmashauri nyingi zimekuwa zikipima na kuuza viwanja kwa matumizi mbalimbali kama chanzo kimojawapo cha mapato kwa halmashauri hizo. Kamati haina kipangimizi juu ya hatua hiyo, hata hivyo inazishauri halmashuri zote nchini kwa kusimamimiwa na Sekretatieti za Mikoa, kuhakikisha kuwa zinafanya zoezi hilo sambamba na kuongeza thamani ya ardhi kwa matumizi mapana ya vizazi vijavyo.

3.4.11 **Mheshimiwa Spika,** sote tunafahamu kwamba, ardhi ya Tanzania haiongezeki ila watu wanaongezeka kila kukicha. Kwa sababu hiyo, Kamati inazishauri halmashauri zote nchini kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi. Mipango hiyo izingatie kutengwa kwa maeneo ya uwekezaji, miji ya kibiashara, makazi

endelevu, maeneo ya viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa, mahospitali na maeneno mengine muhimu.

3.4.12 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inazishauri Halmashauri zote nchini, kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na wadau wa maendeleo, kutenga maeneo maalumu ya ujenzi wa vituo vya teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT Hubs) ili kuweza kufaidika na fursa za kimataifa zinazokuja na uwepo wa ***"mkongo wa taifa wa mawasiliano"***. Uwepo wa mkongo huu na uwepo wa vyuo vinavyozalisha vijana wataalamu wa mambo ya teknohama ni fursa kubwa kiuchumi kama watawezeshwa kufanya tafiti na ugunduzi (tukiigiza mfano wa nchi za Marekani (kule Silicon valley) na China (Shanghai, Beijing na Shenzhen) ambapo wametenga maeneo maalum ya uwekezaji kwenye ugunduzi wa kielektroniki na mawasiliano; si tu wasomi hawa watakuwa wamepata ajira bali wanaweza wakazalisha ajira nyingi zaidi. **Hakuna nchi iliwahi kukuza uchumi wake kwa kutegemea eti serikali ndiye mwajiri mkuu; nchi huendelea panapokuwa na wajasiriamaji wanaobuni na kuanzisha bidhaa mpya.**

3.4.13 Kamati inaamini kwamba, makundi mbalimbali ya kijamii yatanufaika na vituo hivi kwa sababu ya upatikanaji wa elimu na mafunzo mbalimbali na huduma muhimu za kimtandao kwa unafuu. Aidha, vituo hivi vinaweza vikawa na manufaa kwa vijana wetu ambao

wanaweza kufanya kazi kwa fursa zinazopatikana mtandaoni.

3.4.14 **Mheshimiwa Spika,** kamati inaziagiza halmashauri zenye miamba ya Karoo (Karoo rocks) ambayo inasadikiwa kuwa na mafuta, kama zilizopo kwenye mikoa ya Tanga, Dar es salaam, Pwani, Lindi, Mtwara, Rukwa, Kigoma, Katavi na Dar es salaam, kuanza kujipanga ni kwa namna gani watavutia wawekezaji kwenye uchimbaji wa mafuta kwa kutumia teknolojia rahisi na za kisasa, kama ile ya ***horizontal hydraulic factoring***, kwa njia ya ubia *(public private partnership)*, ili sambamba na Serikali kuu kupata hisa na mrabaha wake, halmashauri nazo ziwe na sehemu ya hisa zake kama wabia. Nchi nyingine wamefanya hivyo na wamefanikiwa sana.

## Ushiriki wa Wananchi Katika Mipango na Miradi ya Maendeleo

3.4.15 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inazishauri Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinawashirikisha wananchi kikamilifu katika kutambua fursa walizo nazo ambazo zitachochea ustawi na maendeleo ili kukabiliana na umaskini. Madiwani na Wabunge ambao wamechaguliwa kuwakilisha kundi kubwa la wananchi, wanao uwezo na dhamana ya kuwasimamia watendaji wasiotekeleza majukumu yao kwa maendeleo ya wananchi kwa kushiriki kikamilifu katika vikao vyote na hasa vile vya Kamati za Fedha *(Finance Committees)* na Baraza la Madiwani *(Full Council)*.

3.4.16 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inarudia na kusisitiza kwamba, Sekretarieti za Mikoa ziwe na mipango ya muda mfupi na ya muda mrefu kulingana na mabadiliko ya ongezeko la watu nchini, ili kuepuka tatizo la miundombinu kutokidhi mahitaji halisi na hivyo kusababisha msongamano katika vituo vya kutolea huduma kama vile shuleni, hospitalini, n.k. Pamoja na hayo, Kamati inasisitiza na kuishauri Serikali kuanzisha Mfuko Maalumu wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali za Rufaa kwa kuzingatia kanda za kiutawala ili zitengwe fedha za kutosha kukamilisha miradi mingi kwa muda mfupi.

**Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART)**

3.4.17 **Mheshimiwa Spika,** bila kuonesha ubaguzi wa kutoa vipaumbele vya miradi katika maeneo ya mjini, Kamati inatambua kwamba Jiji la Dar es Salaam ndilo linaloongoza kwa uzalishaji na kwa mapato yatokanayo na kodi inayokwenda moja kwa moja katika Serikali Kuu. Hata hivyo, Jiji hili linakabiliwa na changamoto ya ongezeko kubwa la wakazi na shughuli za kimaendeleo na hivyo kusababisha kuwepo kwa msongamano wa magari. Athari za msongamano huo ni nyingi ikiwemo kuleta hasara kubwa katika uchumi kwa kupunguza saa za kazi *(man hours)* na kuchelewesha watu kwenda kupata huduma za kijamii.

3.4.18 **Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada za serikali na watu binafsi kujenga makazi, ofisi na sehemu za masoko makubwa nje ya jiji, bado tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Ili kupata ufumbuzi wa tatizo la msongamano wa magari jijini Dar es Salaam, mwaka 2007 Serikali ilibuni mradi wa Usafiri wa mabasi yaendayo haraka (Bus Rapid Transit, BRT). Kwa mujibu wa mpango huo, mradi huu ukikamilika inakadiriwa utakuwa umetatua tatizo la usafiri wa umma katika jiji la Dar es salaam na pia kupunguza msongamano wa magari jijini humo mpaka kufikia miaka ya 2030/31.

3.4.19 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza serikali kwa hatua ambayo mradi huu umefikia, na zaidi kwa hatua ya kusainiwa kwa mkataba wa huduma ya mpito. **Niwapongeze sana Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya TAMISEMI kwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa ushiriki wa Watanzania katika utoaji wa huduma ya usafiri unazingatiwa katika hatua za mwanzo na za baadae katika mradi.**

3.4.20 **Kwa namna ya kipekee nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa serikali, Mhe. George Masaju, Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Ndg. Said Mecky Sadick na Mtendaji Mkuu wa DART, Ndg. Asteria Mlambo, kwa kukubaliana na mapendekezo ya Kamati kuwa uendeshaji wa mradi utoe kipaumbele cha kwanza kwa watanzania hususan waendeshaji wa usafiri uliopo sasa (madaladala, UDA na makampuni**

**mengine ya kitanzania) kabla ya kuwakaribisha wawekezaji kutoka nje, na kwamba uwekezaji kutoka nje uwe ni wa kuwaongezea nguvu na kuwajengea uwezo wa kiufundi tu pale ambapo teknolojia hiyo haipo nchini. Ni imani yangu kuwa mradi huu utatekelezwa kwa uzalendo wa hali ya juu.**

3.4.21 **Aidha, kamati inazidi kusisitiza kuwa mradi uanze mara moja na majaribio katika kipindi hiki cha mpito yahusishe uwepo wa mfumo kamili wa kielektroniki wa tiketi unaofanya kazi kikamilifu ili wananchi waone utofauti na wapate motisha ya kutumia mfumo huu na kupaki magari yao nyumbani.**

3.4.22 **Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kuwahamasisha wafanyabishara wa kitanzania wenye nia ya kushiriki katika usafirishaji wa abiria katika Mkoa wa Dar es Salaam kupitia mradi huu, waunganishe nguvu zao na kuumiliki mradi huo wenye thamani kubwa ya pesa. Ifahamike kwamba, huu si mradi wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) wala si mradi wa matajiri wachache katika sekta ya usafirishaji, ni mradi wa Watanzania wote na wadau wa mendeleo katika Jiji la Dar es Salaam.

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

4.1.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, (Mb)

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mhe. Aggrey D. J. Mwanri (Mb) na Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb), Naibu Mawaziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Jumanne A. Sagini, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, na kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

4.1.2 **Mheshimiwa Spika**, vilevile napenda kutoa shukurani za kipekee kwa Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote kwa kuwasilisha vyema taarifa za utekelezaji wa bajeti zilizopita na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

4.1.3 **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukurani kwa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Charles J. Mloka, Wakurugenzi Wasaidizi, Makatibu wa Kamati Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Mwajuma Ramadhan wakisaidiwa na Ndg. Cletty Urassa, kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati wakati wote hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.**

Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb)

**MWENYEKITI**

**Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

Mei, 2015